CBE INTERNATIONAL

# WANAUME, WANAWAKE NA USAWA WA KIBIBLIA.

## WAKRISTO WA USAWA WA BIBLIA

Biblia hufundisha usawa kamili wa Wanaume na Wanawake katika muumbo [Mwanzo 1:26-28, 2:23, 5: 1-2; 1Wakorintho 11:11-12; Wagalatia 3: 13, 28, 5:1].
Biblia hufundisha kwamba Mungu amejethihirisha mwenyewe katika ukamilifu wa maandiko yenye nguvu za neno la Mungu[Mathayo 5:18, Yohana 10:25, 2Timotheyo 3:16, 2Petro 2:21]
Tunaamini yakwamba maandiko lazima yatafusiriwe katika utakatifu na kiini.
Tunatambua tena umhimu wa kufanya tafauti baina ya upuzio na tafusiri: upuzio husiana na msukumo mtakatifu na mwongozo ambapo maandiko yaliyo kubalika kamili ni Neno la Mungu: Tafusiri husiana na shughuli za mwanadamu ambapo tanatafuta kufahamu Ukweli uliothihirika katika mapatano na ukamilifu wa maandiko chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu. Ili kuwa kweli kibiblia wakristo lazima waendelee kuoji imani na mazoea yao chini ya kununzi ya Maandiko.

## Kweli za Biblia

### Muumbo

1. Biblia hufundisha kwamba wote Mwanamume na Mwanamke waliombwa kwa Mfano wa Mungu, walikuwa na uhusiano wa moja kwa moja na Mungu wakigawana pamoja majukumu ya kuzaa na kulea watoto na kuwa na umiliki juu ya taratibu ya muumbo[mwanzo 1:26-28].
2. Biblia hufundisha kwamba Mwanamke na Mwanamume waliuumbwa kwa ukamilifu na usawa wa ushirika. Neno mzaidizi[ezer] linalotumika kuonyesha mwanamke katika mwanzo 2:18 lahusu Mungu zaidi ndani ya utumiaji wa Agano la kale[kwamfano 1Samueli 7:12, Zaburi 121:1-2]. Kwa sababu hiyo, neno hilo halionyeshi maana hasa kwa vyovyote vile kuwekwa chini kwa Mwanamke.
3. Biblia kwamba uumbaji wa Mwanamke kutoka kwa Mwanamume huonyesha asili ya umoja na usawa wa binadamu[mwanzo 2:21-23]. Katika mwanzo 2:18, 20, neno wakufanana naye la maanisha usawa na utoshelevu.
4. Biblia hufundisha kwamba Mwanamume na Mwanamke walishiriki pamoja katika anguko[mwanzo 3:16, Warumi 5:12-21; 1Wakorintho 15:21-22].
5. Biblia hufundisha kwamba, utawala wa Adamu juu ya Hawa ilitokana na anguko na haikuwa mwanzoni sehemu ya taratibu ya uumbaji. Mwanzo 3:16 ni ubashiri wa madhara ya anguko badala ya desturi, taratibu halisi juu ya Mungu.

## Ukombozi.

6. Biblia hufundisha kwamba yesu Kristo alikuja kuokoa Wanawake na Wanaume pia. Kupitia Imani katika Kristo, zote tumepata kiwa Watoto wa Mungu, tumekuwa mmoja katika Kristo, na wariithi za wokovu bila mtajo kwa Taifa, Watu wa kiwango

fulani, au tafuti za kijinsia[Yohana1:12-13;Warumi 8:14-17; 2Wakorintho 5:17; Wagalatia 3:26-28

## Jamii.

7. Biblia hufundisha kwamba siku ya Pentecoste Roho Mtakatifu alikuja juu ya Wanaume na Wanawake Pamoja. Bila tofauti, Roho Mtakatifu hukaa ndani ya wote Wanawake na Wanaume na katika mamlaka hugawa bila upendeleo kuhusu jinsia[ Matendo ya Mitume 2:1-21; 1Wakoritho 12:7, 11, 14: 31]
8. Biblia hufundisha kwamba wote Wanawake na Wanaume wameitwa kukuza vipawa vyao vya kiroho na kuvitumia kama mawakili wa neema ya Mungu[1Petro 4:10-11]. Wote Wanaume na Wanawake wanabarikiwa na vipawa na kuzeshwa kutumikia mwili wote waKristo, chini ya mamlaka yake[Matendo ya Mitume 1:14; 18:26, 21:9; Warumi 16:1-7, 12-13, 15; Wafilipi 4:2-3; Wakolosai 4:15 tazama tena Marko 5:40-41, 16:1-7, Luka 8:1-3, Yohana 20:17-18; fananisha pia mifano ya Agano la kale: Waamuzi 4:4-14, 5:7; 2Mambo ya Nyakati 34:22-28; Mithali 31:30-31, Mika 6:4].
9. Biblia hufundisha kwamba katika uchumi wa Agano Jipya, Wanawake na Wanaume pia walifanya kazi ya Unabii, Ukuhani, na ya Kifalme[Matendo ya Mitume 2:17-18, 21:9, 1Wakorintho 11:5; 1Petro 2:9-10; Ufunuo 1:6, 5:10]. Kwa hivyo Maandishi machache yaliyojitenga yanaonekana kupinga uhuru kamili wa Ukombozi wa Wanawake hayasitahili kutafusiriwa kirahisi na katika hali ya kupinga maandiko matakatifu mengine, isipokuwa utafusiri wa hayo lazima ufanywe kulingana na uhusiano wa hayo na Maandiko mengine na katika ukamilifu wa maana yake[1Wakorintho 11:2-16, 14:33-36; 1Timotheyo 2:9-15].
10. Biblia hueleza kazi ya uongozi kama kuwapa mamlaka wengine katika utumishi badala ya kutumia nguvu yao[Mathayo20:25-28, 23:8; Marko 10:42-45; Yohana 13:13-17; Wagalatia 5:13; 1Petro 5:23].

## Jamaa.

11. Biblia hufundisha kwamba Waume na Wanawake ni wariithi pamoja wa neema katika uhusiano wa mapatano ya utiivu na uwajibikaji[1Wakorintho 7:3-5; Waefeso 5:21; 1Petro3:1-7; Mwanzo21:12]. Kazi ya Mume kama Kichwa[kephale] ni kueleweka kame yule wa upendo wa kujitolea na utumishi ndani ya huu uhusiano wa mapatano ya utiivu[Waefeso5:21-23;Wakolosai 3:19; 1Petro3:7].
12. Biblia hufundisha kwamba wote wakina Mama na Baba wanastahili kuendeleza uongozi katika kukuza, kufunza, kutia nidhamu na kufundisha watoto wao[Kutoka20:12; Walawi 19:3; Kumbukumbu la Torati 6:6-9, 21:18-21, 27:16; Mithali 1:8, 6:20, Waefeso 6:1-4; Wakolosai 3:20; 2Timetheyo 1:5; tazama pia Luka 2:51.

## Welekevu

### Jamii

1. Katika Kanisa, vipawa vya kiroho vya Wanawake na Wanaume vitambuliwe kwa utumishi, na huduma za kufundisha katika viwango vyote vinavyojihuzisha kama; viongozi wa kundi ndogo, washauri, wahimizaji,wasimamizi, mabawabu, watumishi katika meza ya Bwana, wanachama wa halmashauri na katika utunzi wa uchangaji, kufundisha, kuhubiri na kuwabudu.. Kwa kufanya hivi, Kanisa litamheshimu Mungu kama mwanzilishi wa vipawa vya kiroho. Kanisa pia litatimiza amri ya uwakili wa Mungu bila upotevu wa kuogofya katika ufalme wa Mungu ambao unasababisha karibu nusu ya Washiriki wa Kanisa kutengwa kutoka kwa nafasi ya usimamizi.
2. Katika kanisa kutambuliwa wazi kufanyike kwa wote wanawake na wanaume ambao wanafanya kazi ya utumishi na uongozi._Kwa kufanya hivi,kanisa litakuwa kielelezo cha umoja na mapatano ipasayo kueleza jamii ya waumini. Katika ulimwengu ambao umevunjwa na ubaguzi na kutenga,kanisa litajitengwa, kutoka kwa mbinu za kiulimwengu na kiukafiri ambazo zimetungwa kufanya wanawake kujisikia kushushwa chini kwa ajili yao kuwa wake. Hii itasaidia kuzuia hao kutoka kwa katika kanisa au hao kukataa imani ya kikristo.

JAMAA.

3. Katika Nyumbani Mwa Kikristo, Mume na Mke wanapaswa kunyenyekeana kwa mwingine wakitafuta kutimiziana mapendeleo , haja na matarajio ya kila mmoja. Mume au Mke asitafute kumtawala mwenziwe isipokuwa kila mmoja atende kama Mtumishi wa Mwenziwe, katika unyenyekevu akifiria Mwenziwe kuwa bora kuliko yeye. Katika hali yakukwama katika katika kukata kauli imewapasa kutafuta suluhisho kupitia njia za biblia za kusuluhisha mzozo kuliko Mume au Mke kulazimishe uamzi wake kwa Mwenziwe.
   Kwa kufanua hivi, Mume au Mke watasaidia Nyumba ya Kikristo kusimama kinyume cha utumiajia mmbaya wa mamlaka kwa mwenzake na kulinda mji kutoka kwa utukanaji wa mke na mtoto ambao kwa wakati mwingine inasababishwa na mpangilio wa uongozi wa Mume.

4. Katika Nyumba ya Kikristo, Mume na Mke wanapaswa kujifunza jinzi ya kugawanya wajibu wa Uongozi kwa misingi ya vipawa, utendaji, kuweko, na kufikiria juu ya Mwenzake ambaye ameguzwa na uamzi ambao unafikiriwa. Kwa kufanya hivyio Mume na Mke watanjifunza jinzi ya Kuheshimu nguvu na ukamilishaji wao. Hii itazuhia mmoja wao kutokuwa mpotezaji wa siku xote kila mara akilazimishwa kufanya kupendekeza au uongo ili kukinga hathi yao. Kwa kujenga ndoa yao juu ya misingi ya ushirika, mume na mke watakinga nyumba yao kujitenga na maji mafu au ndoa iliyovunika inayotokena na ndoa za kiasil.
5. Katika Nyumba ya Kikristo, wanaume na wanawake amabao hushiriki maisha inayoelezea uhuru ambao wamepata katika kristo watafanya hivyo bila kuwa na mawazo ya hatia au kugeukia unafiki. Wamewekwa huru kutoka kwa tamaduni sizisho za biblia na wanaweza kufurahi katika kuhesabika hao kwa hao katika Kristo.. Katika kufanya hivyo, wataonyesha wazi utiivu wao kwa maandiko, na kuwa mfano kwa wanaume na wanawake wengine wanaotafuta uhuru katika Kristo, na watasimama kinyume cha mitindo ya utawala na kutokuwa na Usawa ambavyo zamani vililazimishiwa Kanisa na Jamaa

Tunaimini yakwamba Usawa wa Biblia jinzi imeonyeshwa katika nakili hii, nikweli kulingana na Maandiko. Tunasimama kwa umoja katika kuamini kwetu yakwamba Biblia katika ukamilifu wake, ni neno la kuweka huru ambalo linatupatia nja bora ya Wanawake na Wanaume kutumia vipawa ambavyo hupewa na Roho Mtakatifu na kwa hivyo kumtumikia Mungu.

Gilbert Bilezikian
Stanley N. Gundry
Catherine Clark Kroeger
Roger Nicole
W. Ward Gasque.
Gretchen Gaebelein Hull
Jo Anne Lyon.

**Christians for Biblical Equality**
122 West Franklin Avenue, Suite 610,
Minneapolis, MN 55404-2426
Phone: **(612) 872-6898**
Email: **cbe@cbeinternational.org**
**www.cbeinternational.org**